**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA SABA**

**Kikao cha Thelathini na Tatu – Tarehe 13 Juni, 2022**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

**MASWALI:**

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

87. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kwa kuwa Fungu la Matumizi katika Wizara zote za Serikali limeundwa kwa sehemu za Unguja na Pemba, na kwa kuwa Hesabu za Mwisho wa Mwaka zinapaswa kujumuisha sehemu zote mbili, na kwa kuwa hesabu kamili ya Fungu la Mapato na Matumizi kwa upande wa Pemba huwa moja kwa moja halionekani, na kwa kuwa kuendelea kutumia mfumo uliopo hivi sasa wa kufunga hesabu kwa njia mjumuishi kunamnyima mtu kupima utendaji wa upande mmoja pekee, na kwa kuwa Baraza la Wawakilishi liliwahi kueleza changamoto zinazozipata wakati wa kutekeleza shughuli zake endapo Serikali itaendelea kutumia mfumo uliopo hivi sasa.

Je, ni hatua zipi zimechukuliwa na Serikali ili kuweza kuwa na Hesabu za Mwisho wa Mwaka ambazo ni Hesabu ya Pemba, Hesabu ya Unguja pamoja na kuwa na Hesabu mjumuisho.

89. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipokea fedha za Maradhi ya Uviko19 na kuzifanyia miradi mbali mbali.

Je, ni ajira ngapi zimepatikana kwa vijana wa Kizanzibari wakati wa utekelezwaji wa miradi hiyo kupitia fedha hizo.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

169. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Imekuwa ni utaratibu usio salama unaoendelea sasa kwa umeme kuunganishwa kupitia mapaani mwa nyumba badala ya kutumia nguzo za umeme. Mfano hai ni nyumba nyingi kuunganishwa kwa mtindo huo katika kijiji cha Pembeni ndani ya jimbo la Pandani.

(a) Je, ni kwa sababu gani umeme huunganishwa kupitia mapaani mwa nyumba badala ya kutumia nguzo za umeme.

(b) Je, ni mazingira yepi yanayoruhusu na yasiyoruhusu kuunganishwa umeme kupitia mapaani mwa nyumba na nani mwenye wajibu wa kuamua matumizi sahihi.

(c) Je, ili kuweza kusambaza umeme nchi mzima katika maeneo yaliyobaki mijini na vijijini kwa sasa, ni nguzo ngapi zinahitajika kwa ujumla wake na zinagharimu kiasi gani.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

154. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Zanzibar ina misitu mingapi ya hifadhi ukitoa Msitu wa Hifadhi ya Taifa wa Ngezi na ule wa Jozani, na imekuwa na tija gani katika kuingizia taifa fedha za kigeni.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

172. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kumekuwa na malalamiko mengi kuhusiana na Serikali kutowajali walimu kwa vitendo na kimaslahi huku ikiwatumia na kuwatumikisha walimu kila panapofanyika shughuli za kitaifa na, kwa maneno ya walimu, wamekuwa wakifanywa chambo na hawana muda wa kutosha wa kupumzika. Zaidi ni kukosa pahala sahihi pa kulalamika kwa sababu Serikali huitumia Wizara ya Elimu ambayo ndio mwajiri wao.

(a) Je, hadi mwezi Machi 2022, ni kiasi gani walimu wanaidai Serikali na itawalipa lini.

(b) Je, kwa nini hakuna utaratibu unaoeleweka na wa usawa wa kulipa stahiki za walimu.

(c) Je, ni lini walimu waliogatuliwa watalipwa madeni yao ya kabla, wakati wa, na baada ya Ugatuzi.

175. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Serikali ililieleza Baraza la Wawakilishi kwamba Skuli ya Maandalizi ya Mlindo ndani ya jimbo la Pandani ambayo ujenzi wake umefikia hatua ya linta tayari imeshakabidhiwa kwa Serikali, kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, na Baraza la Mji Micheweni kwa ajili ya kuikamilisha. Hata hivyo, msimamizi wa ujenzi huo kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDF), Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya jimbo la Pandani, haina taarifa rasmi kuhusu makabidhiano hayo.

(a) Je, ni lini ujenzi wa skuli hiyo ya Maandalizi ya Mlindo utakamilika na kwa gharama gani.

(b) Je, Serikali itamtumia mkandarasi na mshauri elekezi yupi kuukamilisha mradi huo.

(c) Je, katika jimbo la Pandani, ni skuli nyengine zipi ambazo zimepangwa kukamilishwa na Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

<u>**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**</u>

100. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) -

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa kuwa wananchi wa vijiji vya Mgogoni na Tondooni hususan wanafunzi wanaokabiliwa na changamoto ya kwenda na kurudi katika kijiji kimoja wakati wa msimu wa mvua, na kwa kuwa kuna uwezekano mkubwa kwa baadhi ya watoto kupoteza maisha kutokana na kiwango kikubwa cha maji kinachokuwepo baina ya vijiji hivyo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga daraja litakalounganisha vijiji viwili hivi ili kurahisha mawasiliano.

Zanzibar,
13 Juni, 2022.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA